



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MTC/L.10/10/34

Tarehe 18 Agosti, 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

1.0 UTANGULIZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga baada ya kupokea kibali cha ajira Mbadala chenye Kumb Na. **FA.170/367/01"TEMP"/13** cha tarehe **26 Agosti, 2021** kutoka kwa **Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma Na Utawala Bora**, anawatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa zinazohitajika kuomba nafasi wazi Nne (4) kama zifuatazo:

2.0 DEREVA II (4)

2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa waliohitimu kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya udereva ya Daraja E au C1 ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali. Wombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi II watafikiriwa kwanza.

2.2 KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- vi. Kufanya usafi wa gari na
- vii. Kufanya kazi zingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

Mkurugenzi wa Mji, S.L.P.135, Mbinga, Simu Na. +255 (025) 2640664, Nukushi +255 (025) 2640262, Barua Pepe:td@mbingatc.go.tz, Tovuti:www.mbingatc.go.tz


3.0 MAELEZO/ MASHARTI YA JUMLA

- i. Mwombaji awe raia wa Tanzania ambaye ana umri si zaidi ya Miaka 45 na sio pungufu ya Miaka 18
- ii. Barua iambatanishwe na Wasifu binafsi wa mwombaji wa hivi karibuni (Curriculum Vitae) anuani inayotumika, namba ya simu na anuani ya barua pepe (e-mail address) na majina ya wadhamini (referees) watatu wanaofahamika.
- iii. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo vilivyo onyeshwa kwenye nafasi aliyoomba:- Mfano
 - a) Cheti cha utaalamu kulingana na sifa za nafasi husika
 - b) Leseni ya Udereva
 - c) Cheti cha kidato cha nne
 - d) Cheti cha kuzaliwa
 - e) Cheti cha Majaribio ya ufundi (Kama Kipo)
- iv. Matokeo ya muda (provisional/testimonials/statement of results) havitakubaliwa.
- v. Waombaji wawe wenye sifa na uzoefu uliotajwa kwenye tangazo hili la kazi
- vi. Picha 2 ndogo (passport size) za hivi karibuni.
- vii. Waombaji watakaoleta maombi na vyeti vya kugushi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.
- viii. Waombaji wa makundi maalum wanashawishiwa kuomba
- ix. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne vya nje ya nchi vitatakiwa vithibitishwe na NACTE.
- x. Waombaji wenye vyeti vya Astashahada vya nje ya nchi vithibitishwe na NACTE.
- xi. Barua ya muombaji itatakiwa iandikwe kwa Kiswahili au kiingereza.
- xii. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta. Barua zitakazoletwa mkononi hazitapokelewa wala kufanyiwa kazi.
- xiii. **Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 31/08/2021 Saa 9:30 Alasiri.**

Maombi yote yatumwe kwa:-

**Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji wa Mbinga,
S. L. P. 135,
MBINGA**

Imetolewa na:


GRACE S. QUINTINE
**MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI
MBINGA**

**MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI
MBINGA**